**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 04 Juni, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

87. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando)-

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Skuli ya msingi Ukunjwi ni miongoni mwa skuli iliyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo inategemea pia ruzuku kutoka Mamlaka hizi, ili iweze kujiendesha. Vile vile ni skuli ambayo inakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo uchakavu wa majengo na uhaba wa madarasa ya kusomea pamoja na ufinyu wa ofisi ya walimu.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kukabiliana na changamoto hizo.

(b) Je, Wizara imewahi angalau mara moja kuitembelea skuli hii na kuona changamoto zake.

(c) Je, wananchi wa maeneo haya wategemee nini kutoka Serikalini kuhusu maendeleo ya skuli hiyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

59. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na wito mkubwa kwa watumiaji wa benki hasa kipindi hiki cha janga la maradhi ya Corona “Covid 19” duniani, kutumia mitandao katika kupata huduma zao za kifedha, jambo ambalo kwa upande wa Benki zinazotowa huduma ya ATM ya umoja ikiwa ni pamoja na Benki ya PBZ, limekuwa lina changamoto kubwa kwa watumiaji wa ATM hizo.

(a) Je, ni hatua gani Serikali itachukuwa katika kumaliza tatizo la wateja wa PBZ kupata huduma safi za ATM zao badala ya kuhangaika zaidi ya ATM tatu hadi kupata huduma.

(b) Je, ni nini chanzo cha tatizo hili hasa wakati wa mwisho wa mwezi.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

201. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi)
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia nzuri imetoa fedha nyingi kwa ajili ya kuwapatia ajira vijana wake, lakini hadi hivi sasa hakuna hata mradi mmoja ambao unatoa ajira kama ulivyokusudiwa kupitia miradi hiyo ikiwa ni pamoja na “Green House”, maboti na viwanja vya mpira wa miguu.

(a) Je, Wizara itachukua hatua gani juu ya upotevu wa fedha zilizotumika katika kuimarisha miradi hiyo.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kufanya ziara katika Jimbo la Nungwi ili kuangalia miradi hiyo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

192. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Shirika la Taifa la ZSTC katika kuimarisha uzalishaji wa mafuta ya Mimea, liliingia makubaliano na Kampuni ya Kunshan Asia Aroma kutoka nchini China kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda kipya cha kusindika mafuta na ambacho kilishazinduliwa rasmi na aliyekuwa Makamo wa Pili wa Rais wa awamu ya saba. Na kwa kuwa dunia inakabiliwa na janga la maradhi ya Covid 19 (corona) na kiwanda hakijaweza kufanya kazi kutokana na kuwasubiri wataalmu kutoka China

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kiwanda hicho kinaanza kufanya kazi katika kipindi cha muda mchache ujao.

(b) Je, ni kweli kuwa teknolojia iliyotumika katika kiwanda kipya haifahamiki duniani, kiasi cha kushindwa kutafuta wataalamu wengine kwa ajili ya kukifanyia majaribio na kuanza kufanya kazi.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

204. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Serikali ya Awamu ya Saba ilitumia fedha nyingi sana kwa ajili ya ununuzi wa mashine maalum ya kupima vinasaba (DNA) ambayo imekua ikitumika kwa muda sasa na kuwasaidia wananchi wa Zanzibar kupitia huduma hiyo.

(a) Je, ni mara ngapi Serikali imeshaifanyia “service” mashine hiyo tokea ilipoanza kutumika.

(b) Je, ni kiasi gani kwa mwaka kinapaswa kutumika kwa ajili ya kuifanyia “service” mashine hiyo.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

159. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni)
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Moja ya mipango mizuri ya Sera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayotokana na Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2020-2025) ni Uchumi wa Buluu. Hata hivyo, elimu kubwa inahitajika kwa wananchi kufahamu dhana nzima ya Uchumi wa Buluu na mambo wanayohitaji kufanyika ili kuinua uchumi huo.

(a) Je, Wizara imeandaa programu ngapi kwa mwaka kupitia redio na televisheni kwa umma ili kuifahamisha jamii dhana nzima ya uchumi wa buluu.

(b) Je, vikundi vingapi vya vijana vimehamasishwa kuhusu dhana ya Uchumi wa Buluu Unguja na Pemba.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

112. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni)
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa malengo ya msingi ya maji ya mvua pembezoni mwa barabara ni kuyapeleka maji hayo pwani au sehemu maalum iliyotengwa kwa ajili hiyo.

(a) Je, kwa nini mitaro ya maji ya mvua iliyojengwa imeelekezwa katika makaazi ya watu.

(b) Je, hatuoni kuwa kuwepo kwa mitaro hiyo kwenye maeneo hayo, kunawapa hofu na taharuki wananchi wetu kipindi cha mvua.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

172. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo katika kazi zake pia hufanya aina mbali mbali za utafiti wa mazao kwa lengo la kupunguza changamoto zinazowakabili wakulima.

(a) Je, ni aina ngapi za tafiti zilizofanyika na matokeo ya tafiti hizo ni yepi.

(b) Je, ni wakulima wangapi wamefaidika kutokana na tafiti hizo.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**04 Juni, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**